

K.C.S.E 2006 KISWAHILI KARATASI YA 102/3

FASIHI SIMULIZI

1. (a) Fasihi Simulizi ni nini? (alama 2)
(b) Eleza tofauti nne baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. (alama 12)
(c) Nini umuhimu wa Fasihi Simulizi? (alama 6)

TAMTHILIA

Kithaka wa Mberia: *Kifo Kisimani*

2. "Utani? Haukuwa utani! Mtemi amesikia sifa za uzalendo wako.... Mipango yote imepangwa na kupangika. Unafua, bwana, hiari ya binadamu ni kifaa cha mtu mwenyewe. Anaweza kukitumia vizuri au vibaya Anaweza kukitumia kujinufaisha maishani au kujikwamisha njiani. Inategemea mtu mwenyewe."

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 2)
(b) Ni mipango gani inayozungumziwa? (alama 4)
(c) Fafanua jinsi baadhi ya wanajamii wa *Kifo Kisimani* walivyoitumia hiari yao vibaya. (alama 14)

RIWAYA

Z. Burhani: *Mwisho wa Kosa*

3. Linganisha wasifu wa wahusika wafuatao na uonyeshe umuhimu wao katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*:
(a) Monika
(b) Muna

HADITHI FUPI

K. W. Wamitila: *Mayai Waziri wa Maradhi*

Jibu swali la 4 au la 5

Siku ya Mganga

4. "Lakini kulikuwa na tatizo gani iwapo. mganga alikuwa hajui chochote kuhusu ugonjwa?"
(a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 2)
(b) Eleza sifa za mganga anayerejelewa katika hadithi hii. (alama 10)
(c) Taja na ufafanue madhara aliyoyasababisha mganga kwa jamii. (alama 8)

Kachukua hatua Nyingine

5. "Kusema ukweli Mavitu alijua fika kuzichukua hatua."
(a) Thibitisha ukweli wa usemi huu ukirejelea hadithi ya *Kachukua Hatua Nyingine*. (alama 10)
(b) Hatua alizozichukua Mavitu zilikuwa na athari gani? (alama 10)

USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7

6. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

KWELI

1. Neno la kweli daima,
Li nguvu za kutosha
Ni silaha ilo nzima, shahaba kutopotosha
Neno ngome ya hishima, msema kweli hunyosha
La urongo lapotosha, dumu katika ukweli
2. Ukitaka taadhima, na hifadha ya kutosha
Uishi pesye huduma, uwe ndiwe muongosha
Uwe mkweli daima, urongo wako ondosha
La urongo lapotosha, dumu katika ukweli
3. La kweli lina salama, *ghayati* linaridhisha
Lakinga mbele na nyuma, na kati lafurahisha
Hata kesini ungama, Mola atasahalisha
La urongo lapotosha, dumu katika ukweli
4. Ruhusa urongo sema, patatu nakujulisha
Ni kauli ya Hashima, wengi *wamesadikisha*
Ni hadithi twaisoma, nasi tumejifundisha
La urongo lapotosha, dumu katika ukweli
5. Kwanza urongo useme, iwapo wapatanisha
Pili ni mke na mume, ili ndoa kudumisha
Na vitani usikome, ni haki kuhadaisha
La urongo lapotosha, dumu katika ukweli
6. Wasalamu kaditama, sitaki kuyarefusha
Waja wa leo si wema, si hoja kuwagutusha
Wathamini darahima, haki wakaziangusha
La urongo lapotosha, dumu katika ukweli

- (a) Taja manufaa ya ukweli kama yali vyoelezwa na mshairi. (alama 4)
- (b) Taja na kutoa mifano ya tamathali mbili za usemi katika shairi. (alama 4)
- (c) Dondoa na ueleze mifano miwili tofauti ya uhuru wa kishairi katika shairi hili. (alama 4)
- (d) Andika ubeti wa tano katika lugha nathari. (alama 4)
- (e) Eleza maana ya:
 - (i) *ghayati* (alama 1)
 - (ii) *hata kesini ungama, mola atasahalisha*. (alama 2)
 - (iii) *wamesadikisha* (alama 1)

7. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

MKULIMA

Mtazameni..... nguzo ya Afrika
mtumwa wa watumwa waloridhwa!

Amekita jembe lake akilisujudia
Kwa *tambo* liloumbuka na koselehea
Uso ukifuka ukata ulojifanya tabia
na machungu ya maonyu alovumilia.

Moyo wake *maito ulokokomaa* kama kuni
Haujui tena kutarajia wala kutamani
Umekufa ganzi kutohisi raha wala huzuni

Basi tena fikira mambo mukiyafikiri
Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari
Siku ukweli wa hali yake utapodhihiri
Umejiandalia vipi...

huo mkono ulomuumbua na kumkausha
hizo pumzi zilomzimia taa ya maisha
kumfunga kizuizi, gizani *kumtowesha!*

Ni jawabu gani alowekewa na wakati
kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti
kuiliwaza hamaki ya njaa hii ya dhata
Njaa ya maisha itakayo kushibishwa.

- (a) Eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 4)
- (b) Taja na utoe mifano ya aina zozote mbili za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)
- (c) Eleza umbo la shairi hili. (alama 3)
- (d) Onyesha umuhimu wa matumizi ya kihisishi katika shairi. (alama 2)
- (e) Fafanua maana ya:
(i) Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari. (alama 2)
(ii) *kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti*. (alama 2)
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi:
(i) *tambo*
(ii) *ulokokomaa*
(iii) *kumtowesha* (alama 3)